

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII**

Telegrams” “MALIASILI”  
Tel: +255 26 2321514/2321558  
Barua pepe: [ps@maliasili.go.tz](mailto:ps@maliasili.go.tz)  
Tovuti: <http://www.maliasili.go.tz>



Mji wa Serikali Mtumba,  
Mtaa wa Waziri Mkuu,  
S.L.P 1351,  
**DODOMA.**

**TAARIFA KWA UMMA**

**UTEUZI WA MWENYEKITI NA WAJUMBE WA BODI YA WAKALA  
WA HUDUMA ZA MISITU TANZANIA (TFS)**

**Dodoma**, 23 Septemba, 2022

Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Balozi Dkt. Pindi H. Chana (Mb), kwa mamlaka aliyopewa chini ya Kifungu cha 5(1) na 5(4) cha Sheria ya Wakala za Serikali Sura ya 245, amemteua **Brigedia Jenerali Mbaraka Naziad Mkeremy** kuwa **Mwenyekiti wa Bodi** ya Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS). Aidha, amewateua wafuatao kuwa wajumbe wa hiyo:-

1. Dkt. Siima Salome Bakengesa, Mkurugenzi wa Utafiti na Uzalishaji wa Misitu, Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI).
2. Eng. Enock Nyanda Emmanuel, Mkurugenzi Msaidizi – Uchumi na Uzalishaji, Ofisi ya Rais TAMISEMI.
3. Adv. Piensia Christopher Kiure, Mkurugenzi wa Uhusiano, Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB).
4. CPA. Bahati Lucas Masila, Afisa Mwandamizi, Ofisi ya Rais.

Aidha, kwa mujibu wa Kifungu cha 5(5) cha Sheria ya Wakala za Serikali Sura 245, **Prof. Dos Santos Aristariki Silayo**, Kamishna wa Uhifadhi - TFS, anakuwa **Katibu wa Bodi** hiyo.

Uteuzi huu ni wa miaka mitatu kuanzia tarehe 23 Septemba, 2022 hadi 22 Septemba, 2025

Imetolewa na;-

**KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**